# MAJUKUMU, FAIDA NA WAJIBU

1

## Utangulizi

Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu ni mpango kabambe wa taifa wa kuboresha upatikanaji wa dawa muhimu kwa bei nafuu, ubora na huduma ya dawa hasa sehemu za vijijini ambazo hazina kabisa au zina maduka machache sana ya dawa. Uanzishwaji wa mpango huu ulitanguliwa na tathmini ya sekta ya famasia nchini mwaka 2001 na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Bodi ya Dawa (ambayo baada ya sheria ya mamlaka 2003 jukumu hilo lilichukuliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania) ikipata msaada wa kitaalamu kutoka Shirika la Management Sciences for Health (MSH). Tathmini hii ilionesha upungufu wa aina mbalimbali katika utendaji na uendeshaji wa shughuli za maduka ya dawa baridi (DLDB). Upungufu uliojitokeza ni pamoja na: kutokuwepo watoa dawa wenye elimu ya kutosha juu ya utoaji wa dawa, utoaji wa dawa nyeti bila vyeti vya daktari na mazingira yasiyofaa kwa utunzaji na uuzaji wa dawa.

Majaribio ya utekelezaji wa mpango wa DLDM ulianza mwaka 2002, katika Mkoa wa Ruvuma chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Tanzania (TFDA) ikipata msaada wa kitaalamu kutoka MSH. Madhumuni ya mpango huu wa majaribio yalikuwa ni kuzikabili changamoto zilizojitokeza wakati wa tathmini kuhusu utendaji na uendeshaji wa DLDB na kujifunza katika majaribio hayo na kuona uwezekano wa kupanua zaidi mpango huu katika mikoa mingine. Baada ya majaribio ya miaka mitatu na baada ya kufanyika tathmini ya ndani na kisha nje, ilionekana wazi kuwa mpango umefanikiwa kuboresha upatikanaji na ubora wa dawa na huduma kwa ujumla. Mafanikio hayo yalishawishi serikali kupanua utekelezaji wa mpango huu nchi nzima.




*Mafanikio ya mpango wa DLDM katika mikoa ya mwanzo yaliishawishi serikali kupanua mpango huu nchi nzima.*

Hata hivyo, kupanuka kwa mpango huu pekee bila kuweka mikakati au mipangilio madhubuti, haimaanishi kuwa utafanikiwa kutoa huduma bora ambayo itafanya mpango huu kuwa endelevu. Yafuatayo ni maswali ya msingi ambayo yanaukabili Mpango wa DLDM hasa kuhusu uendelevu:

**(i)** Namna gani watoa huduma wa DLDM (wamiliki na watoa dawa) wanaweza kuwezeshwa kushiriki kikamilifu katika kutoa huduma bora ya dawa kwa jamii kwa kufuata sheria, kanuni na viwango kwa hiari yao wenyewe?

**(ii)** Kuzingatia ongezeko la haraka sana la maduka ya dawa muhimu, wamiliki na watoa dawa, utaratibu gani utumike ili kuweza kumshirikisha kila mmoja wao na wadau wengine katika mazungumzo kujadili mambo ya msingi yanayojitokeza kuhusu huduma ya sekta hii?

**(iii)** Namna gani wadau wengine ikiwa ni pamoja na mamlaka husika, wanaweza kufanya kazi pamoja na watoa huduma wa DLDM ili kuhakikisha mpango unakuwa endelevu?

*Uanzishwaji wa vyama vya watoa huduma wa DLDM, ni njia mojawapo ya kuhamasisha usimamizi mahususi miongoni mwa wadau, ili waweze kutoa huduma bora za utoaji dawa kwa jamii.*

Uanzishaji wa vyama vya watoa huduma wa DLDM ni njia mojawapo ya kuhamasisha ufuataji wa sheria, kanuni na viwango kwa hiari ili kuboresha utoaji huduma za dawa, na kuwawezesha kiuchumi ili kufanya mpango wa DLDM uwe endelevu.

## Mantiki

Mnamo Juni 2009, Shirika la MSH likishirikiana na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Tanzania (TFDA) lilifanya upembuzi juu ya vyama vya watoa huduma wa DLDM katika mikoa ya mwanzo ya mpango huu (Ruvuma, Mtwara, Rukwa na Morogoro). Upembuzi ulionesha kuwa watoa huduma walikuwa na sababu tofauti za kuanzisha au kutaka kuanzisha vyama vyao.

*Wakati wamiliki wa DLDM wanalenga zaidi kushughulikia changamoto zinazohusu mfumo, matatizo ya watoa dawa yanahusu zaidi haki za kikazi na kujenga uwezo wao kitaaluma.*

Baadhi ya mambo ambayo wamiliki wa maduka hayo walitaka kuyashughulikia kupitia vyama vyao hivyo ni: uhaba mkubwa wa watoa dawa waliopata mafunzo, jambo ambalo limewafanya baadhi ya wamiliki kufunga maduka yao; kuongezeka kwa madai kutoka kwa watoa dawa ya kutaka mishahara mikubwa na mazingira mazuri zaidi ya kazi; uendeshaji wa huduma ya dawa kinyume na sheria na kanuni za DLDM huku viongozi wa wilaya wakifumbia macho matatizo ya utendaji yanayohusu Bima ya Taifa ya Afya (NHIF), hasa juu ya namna ya kupata malipo ya huduma walizozitoa kwa wanachama wao; matatizo kuhusu ukadiriaji wa kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA); matatizo ya uhaba wa mitaji ya biashara kwa sababu ya masharti magumu ya kukopa kwenye benki; utaratibu usioaminika wa kutawanya madaftari ya dawa kutoka TFDA; ucheleweshaji wa vyeti vya usajili, unyanyasaji na lugha mbaya inayotolewa na baadhi ya wakaguzi wa huduma hiyo. Kwa ufupi, matatizo hayo yote yanaonesha upungufu wa kimfumo ambao unadhoofisha utendaji sahihi wa shughuli zao na kuwafanya wakati mwingine washindwe kukidhi viwango vya huduma vilivyowekwa.

Tofauti na wamiliki wa DLDM, matatizo ya watoa dawa yalihusu hasa ubora wa mazingira ya kazi au haki zao kazini na uboreshaji wa ujuzi wao tofauti na upungufu wa kimfumo. Baadhi ya matatizo yao ni mishahara midogo isiyokidhi hali halisi ya maisha, kucheleweshewa malipo ya mishahara, kutokuwepo kwa likizo, kutokuwa na wasaidizi kwenye maduka, kutokuwa na mpango wa elimu endelevu na kukosa uhuru wa kueleza matatizo yao kwa wamiliki wao wakati wakibaini uvunjaji wa sheria na kanuni unafanyika.

*Vyama vya watoa huduma vinatoa nafasi ya kushughulikia changamoto zitakazosaidia watoa huduma kuendelea kutoa huduma bora za dawa kwa jamii.*

Kutokana na haya yaliyoonekana katika upembuzi huo, imebainika wazi kabisa kuwa kuna sababu ya msingi kutafuta mfumo ambao utakuwa wa kudumu na endelevu utakaoshughulikia matatizo ya wamiliki na watoa dawa. Vyama vya watoa huduma (wamiliki na watoa dawa) wa DLDM vinatoa uwezekano wa kushughulikia matatizo yote ya muundo mzima wa mpango na yale yanayowahusu wamiliki na watoa dawa binafsi kwa lengo la kuboresha huduma na kufanya mpango huu kuwa endelevu kwa muda mrefu ujao.

## Aina ya vyama

Kutokana na tofauti kubwa iliyojionesha katika upembuzi huu kati ya wamiliki na watoa dawa hao, hasa kuhusu mambo muhimu yanayowasibu ambayo wangetaka kuyashughulikia kupitia vyama vyao, upembuzi wa Juni 2009 ulionesha kuwa makundi yote mawili yanahitaji kila kundi kuwa na chama chake. Hali hii imedhihirika kutokana na ukweli kuwa watoa dawa ni waajiriwa wa wamiliki, kwa hiyo chama cha pamoja hakitawapa fursa nzuri ya kushughulikia mambo yao kiuwazi. Hata hivyo, makundi yote mawili yalitambua umuhimu wa vyama vya wamiliki na watoa dawa kufanya kazi pamoja kwa ukaribu zaidi kwa faida ya vyama vyote.

## Majukumu ya vyama

Jukumu la msingi kabisa la vyama vya watoa huduma wa DLDM ni kutengeneza utaratibu kwa wadau hao kufanya kazi pamoja katika kuboresha huduma za dawa kwa jamii na kujiimarisha kiuchumi ili kufanya mpango wa DLDM uwe endelevu.

*Ingawa wamiliki na watoa dawa wanapendelea kuundwa kwa vyama tofauti kushughulikia mambo yao binafsi, makundi yote mawili yanatambua umuhimu wa kufanya kazi pamoja kwa ukaribu zaidi.*

Majukumu maalumu ni pamoja na:

(i) Kuwapa wanachama sauti ya pamoja katika mambo mbalimbali yanayohusu huduma za DLDM;
(ii) Kuwapa fursa ya kubadilishana mawazo, taarifa na uzoefu;
(iii) Kuhamasisha ufuataji wa sheria, kanuni na viwango kwa hiari;
(iv) Kuunganisha na kukusanya nguvu za pamoja katika kufanya kazi kwa lengo kuboresha huduma za dawa na hali ya uchumi ya wanachama;
(v) Kuwawezesha wanachama kukusanya pamoja rasilimali fedha na kuwekeza katika shughuli za kiuchumi;



*Vyama vya watoa huduma wa DLDM vinatoa fursa ya kipekee kwa wanachama kubadilishana mawazo, ujuzi na uzoefu.*

(vi) Kujenga mfumo wa mawasiliano na ushirikiano na wadau wa DLDM ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa, Baraza la Wafamasia, Mamlaka ya Mapato, Serikali ya Mitaa, taasisi za fedha, wafadhili na wengineo;

(vii) Kutetea haki na mahitaji ya wanachama;

(viii) Kutoa nafasi ya kusuluhisha migogoro kati ya watoa huduma wa DLDM wenyewe na mamlaka mbali mbali;

(ix) Kusaidia wanachama kuongeza mitaji kwa kuwaunganisha na taasisi za fedha na kuwadhamini wakati wanachukua mkopo kwenye taasisi hizo;

(x) Kuwawakilisha wanachama kwenye vikao vinavyohusu shughuli za DLDM katika ngazi mbalimbali.

## Faida

Chama cha watoa huduma wa DLDM kinachoendeshwa vizuri, kina uwezo wa:-

- Kutetea kikamilifu haki na mahitaji ya wanachama kwa kuwapa sauti ya pamoja katika shughuli za DLDM;
- Kuimarisha uhusiano mzuri wa kikazi kati ya watoa huduma wa DLDM;
- Kuwawezesha wanachama kiuchumi;
- Kuimarisha ufuatiliaji wa sheria, kanuni na viwango kwa hiari ili kuboresha utoaji huduma;
- Kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa ndani na wa kitaasisi ili kuboresha na kuendeleza huduma za dawa;
- Kuimarisha uendelevu wa mpango wa DLDM.

*Jukumu la msingi la vyama vya watoa huduma wa DLDM ni kuwapa wanachama fursa ya kufanya kazi kwa pamoja, katika kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili utoaji huduma za DLDM na pia kuwajengea uwezo wa kitaalamu na kiuchumi ili kufanya mpango wa DLDM uwe endelevu.*

### *(i) Kuwapa sauti ya pamoja watoa huduma wa DLDM*

Vyama vya watoa huduma wa DLDM vinaweza kuleta faida kubwa sana kwa wanachama wake kwa kuwapatia uwanja ambapo kwa sauti moja wanaweza kusimamia mahitaji na malalamiko yao.

Kwa watoa dawa ambao wanaona kuwa mazingira yao ya kazi hayazingatii haki zao za msingi kama vile mishahara inayokidhi mahitaji yao, nafasi ya likizo, muda unaofaa wa kazi na uhusiano mzuri wa kikazi na wamiliki wa DLDM; chama cha watoa dawa kinawapatia fursa nzuri ya kutoa malalamiko yao kwa njia ambayo

haiwezi kupuuzwa na wanaohusika. Chama hicho pia kinaweza kuwa msaada mkubwa katika kupigania mahitaji mengine ya watoa dawa hao kama vile mafunzo ya mara kwa mara na mafunzo endelevu ili kuendeleza ujuzi wao wa kazi.

*Vyama vya watoa huduma vina uwezo wa kupigania mahitaji ya wanachama, kuimarisha uhusiano kati ya watoa huduma wa DLDM ili kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii*

Kwa upande wa wamiliki, chama kinawapa pia fursa ya kuzungumza kwa sauti moja kuhusu upungufu uliopo katika mfumo mzima wa mpango wa DLDM, ambao unawakwaza katika jitihada zao za kujiwezesha kiuchumi na kuboresha huduma za dawa kwa jamii.

### *(ii) Kuimarisha uhusiano wa kikazi kati ya watoa huduma wa DLDM*

Uhusiano mzuri wa kikazi kati ya wamiliki na watoa dawa ni muhimu katika kurahisisha utendaji wa kazi katika maduka hayo. Ifahamike wazi kuwa kila mmoja anamuhitaji mwenzake ili kufikia azma yao ya kiuchumi na kuhakikisha wanatoa huduma bora ya dawa kwa jamii wanayoihudumia. Vyama hivi vinaweza kuwa kichocheo cha kujenga uhusiano mzuri na imara wa kikazi kati ya makundi haya mawili kwa kuunda utaratibu wa kushughulikia matatizo ya kikazi yanayowakabili, na kujenga makubaliano katika mambo ambayo yanaweza kuleta usumbufu katika utendaji. Kati ya vitu vya msingi vinavyoweza kuzungumzwa kati ya mmiliki na mtoa dawa ni; mazingira ya kazi kwa mtoa dawa, mishahara na marupurupu, tabia za mtoa dawa na ufuataji wa sheria, kanuni na viwango hasa pale mmiliki anapojaribu kupuuza ushauri wa kitaalamu kutoka wa mtoa dawa. Kuwa na chama kutasaidia kuboresha uhusiano kati ya wadau hao ili kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii na kuimarisha biashara hii.

### *(ii) Uwezeshaji kiuchumi*

Chama cha watoa huduma wa DLDM kinaweza kuwawezesha wanachama kiuchumi kwa:

*Uhusiano mzuri wa kikazi kati ya wamiliki na watoa dawa ni muhimu ili kuleta ufanisi katika maduka ya dawa.*

- Kuwapa fursa ya kukusanya pamoja rasilimali fedha ili kuwekeza katika shughuli za kiuchumi;
- Kushawishi taasisi za fedha kutoa mikopo kwa masharti nafuu kwa wanachama wao;
- Kuwapa fursa ya kuanzisha ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS) ambazo zitakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi kufanikisha mahitaji yao ya kifedha;
- Kujenga uwezo wa kufanya ununuzi wa pamoja wa dawa na bidhaa nyingine zinazoweza kuwekwa kwenye maduka hayo, na kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza faida kutokana na kununua kwa wingi kwa mara moja;
- Kushawishi mamlaka husika kupanua orodha ya dawa na bidhaa nyingine zilizoidhinishwa kulingana na mabadiliko ya mahitaji ya jamii inayopewa huduma;
- Kushawishi mamlaka husika kuhusu kuboresha masharti ya ulipaji kodi ili hasa kwa watoa huduma wa DLDM ukizingatia manufaa makubwa ya kijamii yanayotokana na huduma za DLDM.



*Vyama vya watoa huduma vinatoa nafasi ya kufanya manunuzi ya pamoja ya dawa na bidhaa nyingine zilizo katika maduka ya dawa, kwani kwa kufanya hivyo hupunguza gharama za uendeshaji na kupata faida zaidi.*

### *(iv) Kuimarisha ufuataji wa sheria, kanuni na viwango kwa hiari*

Vyama vya watoa huduma vinaweza kusaidia kuboresha ufuataji wa sheria, kanuni na viwango kwa:-

- Kuwahamasisha wanachama kufuata sheria, kanuni na viwango vilivyowekwa na mamlaka husika;
- Kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wanachama ambao wanaendesha biashara yao kinyume cha sheria na taratibu kwa kutoa taarifa kwa mamlaka inayohusika;
- Kuwafuatilia maofisa wa halmashauri na wakaguzi ambao wanashirikiana na watoa huduma ambao wanafanya shughuli zao kwa kuvunja sheria au taratibu na kuharibu sifa na ubora wa huduma wa sekta nzima;
- Kushirikiana na idara ya afya ya halmashauri kusimamia shughuli za maduka ya dawa muhimu. Baadhi ya halmashauri zimekwishaonesha utayari wa kushirikiana na vyama hivyo katika kufanya shughuli za usimamizi;
- Kushirikiana na mamlaka husika ili kusaidia upatikanaji wa vitendea kazi kwa wanachama kwa karibu zaidi na kwa urahisi. Kwa mfano, vyama vinaweza kutumika kusambaza daftari la dawa kwa wanachama wote wilayani badala ya TFDA kutegemea kitengo cha afya cha halmashauri kusambaza daftari hilo;
- Kufanya kazi pamoja na mamlaka husika katika kushughulikia changamoto za kimfumo kama vile upungufu wa watoa dawa na ukosefu wa mafunzo ya mara kwa mara na endelevu.

*Vyama vya watoa huduma wa DLDM vina jukumu muhimu la kuhamasisha ufuataji wa sheria, kanuni na viwango kwa hiari.*

### *(v) Kuimarisha uhusiano wa kitaasisi*

Vyama vya watoa huduma vinatoa fursa nzuri ya kuunganisha wanachama wake na taasisi zifuatazo:-

- Mamlaka ya Chakula na Dawa na Baraza la Wafamasia katika kushughulikia changamoto ambazo zinakuwa vikwazo katika shughuli za utoaji huduma bora za DLDM;
- Taasisi za fedha kushughulikia mahitaji ya kifedha/mitaji ya biashara;

- Taasisi za mafunzo kwa ajili ya msaada wa mafunzo ya biashara kwa wamiliki wa maduka na watoa dawa wa huduma hiyo;
- Mamlaka za halmashauri ya wilaya ili kufanikikisha ushirikiano katika mipango na bajeti za halmashauri.
- Wafadhili na wadau wengine wa maendeleo kwa kupata msaada wa kitaalamu na kifedha kwa vyama hivyo;
- Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika kushughulikia utozaji wa kodi.
- Bima ya Afya ya Taifa katika kushughulikia matatizo ya kiutendaji ikiwa ni pamoja na ulipwaji wa madai kwa huduma iliyotolewa kwa wateja wake;

*Vyama vya watoa huduma vina uwezo wa kuwaunganisha wanachama na taasisi mbalimbali, na wadau wengine ili kupata msaada wa kiufundi na kifedha.*

### *(vi) Kuimarisha uendelevu wa mpango wa DLDM*

Kwa kusimamia mahitaji ya wamiliki na watoa dawa wa DLDM, kuimarisha uhusiano mzuri wa utendaji wa shughuli kati ya wamiliki na watoa dawa na wadau wengine, kuhimiza usimamizi wa kisheria na kufuata viwango vilivyowekwa kwa hiari yao wenyewe, kuimarisha uhusiano mzuri na taasisi mbalimbali na kuwawezesha kiuchumi wamiliki na watoa dawa. Vyama hivyo vina wajibu mkubwa wa kuhakikishia utoaji wa huduma bora za dawa kwa jamii kwa njia endelevu.



*Baadhi ya halmashauri zimeonesha utayari wao wa kuhusisha vyama vya watoa huduma wa DLDM katika shughuli za ufuatiliaji wa maduka ya dawa muhimu.*

## Wajibu

Zaidi ya vyama hivi kuwa mstari wa mbele katika kulinda maslahi ya wanachama, pia vina majukumu mengine kama:-

- Kuhakikisha utoaji wa huduma bora ya dawa kwa jamii kwa kuhamasisha ufuataji wa sheria, kanuni na viwango kwa hiari;
- Kulinda afya za wateja kwa kuhamasisha matumizi ya bora ya dawa na ununuzi wa dawa kutoka kwa wasambazaji waliosajiliwa;
- Kuwalinda wateja dhidi ya huduma zisizojali maslahi ya wateja kama vile kupanga bei ya dawa isiyozingatia uwezo wa wateja unaofanywa na watoa huduma wa DLDM wasio waaminifu;
- Kuilinda sekta ya DLDM dhidi ya wasimamizi wa sheria wasiofuata kanuni na taratibu zilizowekwa kwa maslahi binafsi.
- Kujenga na kuendeleza hadhi ya sekta kwa kuhamasisha uwazi na uwajibikaji kwenye shughuli zote za DLDM.




*Vyama vya watoa huduma vina jukumu la kulinda afya za wateja wao kwa kuwapa maelekezo ya matumizi mazuri ya dawa na kununua dawa kutoka kwa wasambazaji wa kuaminika.*

*Imetolewa na Shirika la Management Sciences for Health (MSH) kwa ushirikiano na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).*
*Utayarishaji na usanifu wa kitini hiki umefanywa na Shirika la Medianet Ltd.*
*Shukrani za pekee ziwaendee Rockefeller Foundation kwa msaada wa kifedha.*